Salamu kwa Familia ya Wilaya ya Shule ya Kaunti ya DeKalb,

Tumeshuhudia katika wiki, miezi, miaka na miongo kadhaa iliyopita jinsi ubaguzi wa rangi na kutovumiliana kumeathiri jamii ya Watu Weusi na jamii zingine za rang. Kesi ya Derek Chauvin imekasirisha na kuhuzunisha mioyo ya wengi, wakati wote huu bado tukiendelea kupambana na janga la ulimwengu.

Ni matumaini yangu kuwa hukumu hio italeta mabadiliko chanya katika mifumo yetu ya kiserikali na jamii. Wilaya ya Shule ya Kaunti ya DeKalb (DCSD) inasherehekea utofauti wa watu wake, na hatupaswi kupoteza mwelekeo wa sifa hii muhimu kwa sababu ya vitendo vya wachache. Niwahimiza waalimu, wafanyakazi, wazazi na walezi wetu kuchukua wakati wa kuzungumza na wasomi wetu na kuwasaidia kuelewa maana ya tukio hili.

## Mpango wa Masomo ya Msimu wa Kiangazi wa MOSAIC

Usajili sasa umefunguliwa kwa Mpango wa Wilaya wa Masomo ya Msimu wa Kiangazi wa MOSAIC. Mpango huu unasaidia msingi wa mafundisho wa wilaya ya shule—wanafunzi wetu, walimu wetu, na maudhui yanayofundishwa na kujifunza —kupitia masomo ya urekebishaji, uongezaji kasi, uboreshaji, na kihisia na kijamii. Lengo letu ni kuwashirikisha wanafunzi wote ikiwa ni pamoja na wanafunzi wa Kiingereza, wanafunzi wenye ulemavu, na wanafunzi wenye vipawa.

Kupitia masomo ya ana kwa ana, mahuluti na ya mtandaoni, wanafunzi watafaidika na mafundisho yanayoongozwa na mwalimu na masomo yaliyoelekezwa na wanafunzi ambayo ni ya kukusudia. Wanafunzi watashiriki katika hali halisi, jumuishi na muhimu.

Tafadhali bofya hapa ili kujisajili.

| MPANGO | HADHIRA | TAREHE ZA MPANGO | MUUNDO |
|---|---|---|---|
| Urejeshaji Alama wa FLEX | Wanafunzi wa Gredi ya 8 wanaofanya kozi za HS pekee na Wanafunzi wa Gredi za 9-12 | Juni 1 – Juni 17 | Mtandaoni katika Wilaya Yote |
| Darasa za Kwanza za FLEX | Wanafunzi wa Mwaka wa Mwisho | Juni 1 – Juni 24 | Mtandaoni katika Wilaya Yote |
| Ufidiaji wa Alama wa Shule ya Upili | Wanafunzi wa Gredi ya 8 wanaofanya kozi za HS pekee na Wanafunzi wa Gredi za 9-12 | Juni 1 – Juni 30 (Inategemea) | Mahuluti katika Shule ya Eneo |
| Kambi ya Mpito Kati ya Shule ya Upili na Chuo kwa AP | Gredi 9-12 | Wiki ya 1 katika Julai | Mahuluti katika Shule ya Eneo |
| Kambi ya Mpito Kati ya Shule ya Upili na Chuo ya Msimu wa Kiangazi | Wanafunzi wanaokamilisha gredi za 6 na 9 | Julai (Inategemea) | Mahuluti katika Shule ya Eneo |
| Mwaka Ulioongezwa kwa Elimu Maalum | Wanafunzi wa Elimu Maalum (Pre-K-12) | Juni 7 – Julai 16 | Mahuluti katika Wilaya Yote |
| Mpango wa Chuo cha Wasomi (Scholars Academy) | Gredi 3-8 | Juni 7 – Juni 30 | Mahuluti katika Shule ya Eneo |
| Serendipity | Gredi 1-6 | Juni | Mtandaoni katika Wilaya Yote |
| Mipango ya Uboreshaji katika Shule za Title I | Gredi K-12 Safari za Masomo | Julai | Mahuluti katika Shule ya Eneo |
| Kambi ya Ujuzi wa Kusoma na Kuandika | Gredi K-2 | Juni 7 – Juni 30 | Mahuluti katika Shule ya Eneo |
| Mpango wa My Brother's Keeper | Wasomi Wanaofadhiliwa na MBK | Juni 28 – Julai 2, 2021 | Mahuluti katika Wilaya Yote |
| Kambi ya Ufundi wa Vyombo vya Hewa | Gredi 4-6 | Juni 21 – Julai 2, 2021 | Mahuluti katika Wilaya Yote |
| STEM pamoja na Ujuzi wa Kusoma na Kuandika | Gredi 6-8 | Julai 19 – Julai 29, 2021 | Mahuluti |

| Mpango wa Uboreshaji wa CTAE | Inategemea | Juni/Julai | Mahuluti |
|---|---|---|---|
| Safari za Masomo (Uboreshaji wa Ujuzi wa Kusoma na Kuandika) | Gredi za Pre-K hadi 2 | Juni – Julai | Nyumbani |
| Kanusho: Fursa za masomo ya msimu wa kiangazi kwa uboreshaji, urekebishaji, ufidiaji wa alama, na uongezaji kasi ya kusoma hutegemea mwongozo wa hivi karibuni wa jimbo, eneo na wilaya kuhusiana na ushauri wa afya wa COVID-19. Tarehe zinaweza kubadilika. | | | |
| Vidokezo:<br>• Mipango ya ana kwa ana itawezeshwa kupitia vikundi vidogo vyenye uwiano wa mwanafunzi na mwalimu wa 1:15.<br>• Mipango mahuluti itajumuisha vikao vya mtandaoni na vya ana kwa ana. | | | |

**Mwaka wa Shule wa 2021-2022**

Huku Wilaya ikifanya mipango ya mwaka wa shule wa 2021-2022, tunazingatia mahitaji ya wanafunzi na waalimu wetu. Ni muhimu tuendelee kuzingatia matokeo ya wanafunzi na kufanya mipango ya siku 5 za masomo ya wakati wote, ya ana kwa ana kwa wanafunzi wote katika mwaka ujao. Ingawa wilaya inazingatia masomo ya ana kwa ana, tunafurahia pia kupanua Chuo cha FLEX ili kutoa masomo ya mtandaoni kwa mbali kama chaguo kwa wanafunzi wa shule ya kati na sekondari. Chaguo la masomo ya mtandaoni litakuwa nyongeza ya chuo cha FLEX lakini litakuwa limeunganishwa na kila shule ya nyumbani.

Katika juhudi za kukusanya maoni na mawazo kutoka kwa jamii yetu ya DCSD kuhusu mwaka wa shule wa 2021-2022, tutaandaa mikutano ya kutoa maelezo ya eneo/jamii mnamo tarehe 27-29 Aprili. Tafadhali weka alama kwenye kalenda yako na upange kuhudhuria mikutano ya mtandaoni, kulingana na ratiba iliyo hapo chini.

Bofya kwenye eneo ili kuhudhuria mikutano ya mtandaoni.

| Eneo | Msimamizi wa Elimu wa Eneo | Tarehe | Saa |
|---|---|---|---|
| Eneo la 1 | Bi. Melanie Pearch | 27-Aprili | 06:00 |
| Eneo la 2 | Bw. Trenton Arnold | 28-Aprili | 06:00 |
| Eneo la 3 | Dak. Sean Tartt | 29-Aprili | 06:00 |
| Eneo la 4 | Dak. Antonette Campbell | 29-Aprili | 06:00 |
| Eneo la 5 | Dak. Triscilla Weaver | 27-Aprili | 06:00 |
| Eneo la 6 | Dak. Candace Alexander | 29-Aprili | 06:00 |
| Eneo la 7 | Dak. Rodney Swanson | 29-Aprili | 06:00 |

**Mpango wa Wanafunzi wa Kiingereza**

DCSD inaendelea kushirikiana na jamii yetu ya kimataifa. Wilaya imejitolea kuhakikisha kuwa familia za Wanafunzi wetu wa Kiingereza zinapewa rasilimali muhimu ili wasomi waweze kufaulu na kufanikiwa.

Ili kuendelea kujenga mpango madhubuti wa ELL, wilaya itapeperusha kipindi cha kwanza cha runinga na redio cha Kihispania kupitia *La Vision*. Kipindi hiki cha kila mwezi kinaweza kutazamwa kwenye La Vision Radio na Facebook.

Wilaya pia itashiriki katika Mkutano wa ELL pamoja na wajumbe ambao watajadili mikakati ya mawasiliano, ushiriki wa familia, na huduma za usaidizi katika siku ya shule. Mbali na kuandaa mikutano ya kila mwezi ya kushiriki maelezo pamoja na jamii yetu ya kimataifa; wilaya itakuwa mwenyeji wa tamasha la kimataifa wilayani kote katika msimu huu wa kiangazi.

Tunatazamia kusherehekea familia za Wanafunzi wetu wa Kiingereza!

**Georgia Milestones**

Mwezi huu umekuwa mwezi muhimu kwa wanafunzi wetu wengi wanapofanya mtihani wa Mwisho wa Daraja wa Georgia Milestones. Ningependa kuhimiza wanafunzi wetu wote kufanya bidii! Usiogope mtihani. Kumbuka nukuu hii kutoka kwa Dk. Benjamin Spock, “Jiamini, unajua zaidi ya unavyodhani.”

**Siku ya Dunia**

Mnamo tarehe 22 Aprili, DCSD iliadhimisha Siku ya Dunia kupitia shughuli nzuri kwa wanafunzi, kupitia Kituo cha Sayansi cha Fernbank na Huduma zetu za Lishe. Natumai kila mtu alichukua wakati kufanya maalum kwa sayari yetu, kama vile kupanda bustani au mti, kutoa pipa la urejeshaji, au kutembelea soko la wakulima la eneo ili kununua matunda au mboga mpya. Lazima tuchukulie kila siku kama Siku ya Dunia!

**Siku ya Wataalamu wa Usimamizi**

Mnamo tarehe 21 Aprili, tulisherehekea wasimamizi wetu wa kushangaza katika wilaya nzima. Ningependa kuwashukuru wataalamu wote wa usimamizi kwa kazi mnayofanya. Mafanikio ya wilaya yetu ni dhihirisho la bidii na kujitolea kwenu. Asante! Hatungeweza kufanikiwa bila ninyi!

Kuwa na wiki njema!